**Maswali na Majibu**

1. Yesu alifundisha watu juu ya nini?
   *Yesu alifundisha juu ya wokovu wa Mungu na Ufalme wake.*
2. Taja tabia 5 zenye Yesu alisema tuwe nazo ili tumfurahishe Mungu.
   *Maskini wa roho, huzunikia dhambi, upole, njaa ya haki, rehema, moyo safi, wapatanishi teswa kwa ajili ya imani.*
3. Mfano wa hadithi ni nini?
   *Ni hadithi inayofudisha juu ya somo.*
4. Yesu alifundisha sisi nini alipopeana mfano wa barabara mbili?
   *Barabara safi, pana inaelekeza mautini. Barabara nyembamba, ngumu inaelekeza kwa Ufalme wa Mungu.*
5. Katika hadithi ya Yesu, nani alisaidia mtu aliyejeruhiwa na wanyan'ganyi?
   *Msamaria ndiye alisaidia mtu aliyejeruhiwa.*
6. Hadithi ya Msamaria mwema inatufunza nini?
   *Kwamba ni lazima tuwe wazuri na tusaidie yeyote anayehitaji.*
7. Eleza hadithi ya nyumba mbili.
   *Mtu mmoja alijenga kwa mwamba na mwingine akajenga kwa mchanga. Dhoruba ilipokuja, nyumba iliyokuwa kwa mchanga ilianguka chini lakini iliyokuwa kwa mwamba ilikaa ngumu.*
8. Huu mfano unatufundisha nini?
   *Tujenge maisha yetu kwa mafundisho ya nguvu ya Yesu.*
9. Ni nani tunapaswa kumpa nafasi ya kwanza, nani ya pili na nani ya tatu?
   *Mungu kwanza, wapili ni wenzetu, sisi wenyewe mwisho.*
10. Mungu anajua wakati mashomoro inaanguka chini. Hiyo inatufundisha nini?
   *Sisi ni watoto wa Mungu. Anatujua na anatulinda kwa shida zetu zote.*

## Mistari ya kukariri

Mathayo 5:3 – 10; Mathayo 5:14 – 16; Mathayo 6:26 na 32

## Mazungumzo

Tafuta mafundisho ya Yesu kutoka kwa Mathayo 5:1 – 16. Zungumza juu ya maana ya kila tabia na vile tunaweza kuonyesha kwa haya maisha yetu.

## Kuandika

Mbona Yesu alikuwa akifundisha kwa mifano? Andika juu ya mfano mmoja wa Yesu na maana yake.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 33 Mafundisho ya Yesu

**SOMA Mathayo 5:1 – 10 na 13 – 16; 7:13 – 14 na 24 – 27; Luka 10:29**

**SOMO**

Yesu alikuja kutimiza ahadi za Mungu zote. Alikuja kuleta wokovu kwa watu wote hata wa mataifa. Yesu alifundisha watu kwa miaka mitatu. Aliwafundisha juu ya wokovu wa Mungu. Aliambia watu juu ya Ufalme wa Mungu utakaosimamishwa hapa duniani. Yesu aliwambia kwamba ikiwa wanataka kuwa kwa Ufalme wa Mungu, lazima wapende Mungu na kuishi maisha yanayompendeza.

Yesu alifundisha kwamba watu wanatakiwa wabadilishe njia zao na hata tabia. Sheria zenye Mungu alimpa Musa zilihitaji watu wajue tofauti kati ya mabaya na mazuri. Sheria zilikuwa ni masharti zilizotungwa ili zitimizwe. Yesu alifanya sheria zikawa na nguvu zaidi. Alionyesha watu sheria ya upendo. Alifundisha kwamba lazima watu wawe na haja ya kufanya mazuri, kuonyeshe upendo wao kwa Mungu. Lazima wazuie mawazo yao na mienendo yao kutokana na mabaya. Lazima watu wampende Mungu na wenzao kuliko kujipenda wenyewe.

Yesu alifundisha kwamba Mungu anataka tuwe watoto wake. Mungu anatupenda na ametupa vitu vingi sana. Lazima tuonyeshe upendo wa Mungu kwa watu wengine. Hii ina maana kwamba tusipende tu familia zetu na marafiki wetu. Ina maanishe tuwe wazuri kwa kila mtu. Yesu alituonyesha mfano mzuri sana wa kuishi kama watoto wa Mungu. Yesu alikuwa mzuri kwa kila mtu aliyekutana naye. Alisamehe waliokuwa wabaya kwake. Yesu hakukuwa mchoyo. Wakati wote aliweka Mungu na watu wengine kwanza. Yesu alishinda majaribu yote. Aliishi maisha yasiyo na mawaa. Maisha yake yaliyokuwa kamilifu aliyaweka msalabani kama dhabihu. Alikufa ili tusamehewe dhambi zetu. Alikufa ili tuwe na tumaini la wokovu. Lazima tuige na tujaribu kuishi maisha bila mawaa.



Yesu alisema kwamba Mkristo lazima awe kama chumvi, inayofanya chakula kuwa na ladha. Lazima aonyeshe mfano mzuri kwa wale unaoishi nao. Mkristo lazima awe kama taa inayowaka ili kuonyesha kuishi vizuri. Lazima aonyeshe mwenendo wa Mungu na upendo kwa wenzake.

Yesu alifundisha eti mtu yeyote anayependa Mungu, atakuwa na furaha na kubarikiwa. Aliwambia vile Mungu anataka wawe watu wa namna gani.

| | |
|---|---|
| **Maskini wa roho** | - watu wasioamini kwa utajiri, lakini wanaamini Mungu, walio wapole na wanatafuta rehema ya Mungu. |
| **Huzuni** | - watu wasio na furaha kwa ajili ya dhambi na kifo. |
| **Upole** | - watu wasiotembea kwa njia zao wenyewe ila kwa njia za Mungu |
| **Njaa na kiu cha haki** | - watu wanaotamani kujua na kufanya yaliyohaki |
| **Rehema** | - watu wanaosamehea wengine |
| **Moyo safi** | - watu wasiofanya wala kufikiri maovu |
| **Patanisha** | - watu wanaofundisha wenzao kuishi kwa amani, bila wivu wala chuki |
| **Teswa kwa haki** | - watu waliokubali kuumia kwa ajili ya imani yao |

Hivi ndivyo Yesu alikuwa. Lazima tujaribu tuwe kama yeye. Ni vigumu kuwa na sifa hizo. Ni sifa yenye haitakusaidia kufaulu kwa maisha ya sasa wala kukubaliwa na watu wa hii dunia. Lakini zawadi ya kufurahisha Mungu ni kubwa mno – kuitwa wana wa Mungu, kupata matarajio yetu kwa Ufalme wa Mungu. Inatupasa tufanye bidii na tumfuraishe Mungu. Inatupasa kuomba Mungu, tusome neno lake kila wakati ili litusaidie.

Yesu alisema kwamba sio rahisi kufuata mafundisho yake. Tena sio rahisi kuishi kama watoto wa Mungu. Wengi wao hata hawatajaribu. Yesu aliwambia kwamba, maisha ni kama barabara mbili. Barabara moja ni nyembamba, si nyororo na ina mwinuko. Watu wachache wanaitumia. Hii barabara ni barabara ya uzima. Inatuelegeza kwa Ufalme wa Mungu. Halafu kuna barabara ingine. Ni pana na haina shida kuifuata. Watu wengi wanaendea hiyo barabara. Lakini barabara nyepesi hii inaelekea kwa kifo. Hata njia iwe ngumu namna gani, tumfuate Kristo ili tuende kwa Ufalme wa Mungu.

Yesu alisema hadithi ya mtu aliyekuwa barabarani akienda Yeriko kutoka Yerusalemu na akashambuliwa na wanyan'ganyi. Aliachwa kando ya barabara ili afe. Kuhani alikujia hiyo barabara lakini hakusaidia yule mtu. Alipitia upande mwingine wa barabara na kuenda. Baadaye Mlawi naye alikujia hiyo barabara. Akaona yule mtu aliyepigwa. Alipita kando upande mwingine wa barabara na akaenda zake.



Mwishowe alikuja Msamaria. Wasamaria walikuwa adui na Wayahudi. Lakini vile aliona yule mtu Myahudi amejeruhiwa, alimhurumia, akamfunga vile vidonda kwa vitambaa na kumpeleka kwa nyumba ya wageni na kumsaidia zaidi. Akalipia ulinzi wake kwa hiyo nyumba ya wageni mpaka atakapopona.

Yesu aliuliza, "Nani ndiye jirani kwa mtu aliyejeruhiwa?" Yesu alikuwa anafundisha kwamba tusaidie mtu yeyote aliye na shida hata kama hatumpendi. Jirani ni mtu aliye na mahitaji si yule unayeishi naye karibu. Jirani ni mtu anataka tumsaidie. Mungu anatupenda sana. Inabidi hata nasi tuonyeshe huo upendo kwa wenzetu. Tusipite wale watu wanaohitaji tukiweka vijisababu kwamba tumechoka au tuko na shuguli zingine.

Yesu alikuwa mfano mzuri sana wa Msamaria Mwema. Alijali watu wengi sana alipokuwa hapa duniani. Yesu hakuchoka wala kusema kwamba ana shuguli nyingi na akatae kusaidia yeyote aliyekuja kusaidiwa. Sisi ni kama yule mtu aliyejeruhiwa. Tunamajeraha ya dhambi na tuko barabarani tunaelekea mautini. Yesu anatukujia. Anajitolea kutusameha dhambi zetu na atupeleke kwa Ufalme wa Mungu.

Yesu alisema hadithi ya watu wawili waliojenga nyumba kila mtu yake. Mtu wa kwanza alijenga kwa msingi mzuri sana wa mwamba. Alifanya bidii sana, akajimba mpaka ndani ili ajenge kwa msingi wa mwamba. Nyumba yake ilisimama imara bila kutikisika kwa gharika wala dhoruba. Mtu wa pili alijenga nyumba yake haraka haraka bila kujali. Alijenga kwa mchanga. Dhoruba ilipokuja, hiyo nyumba ilianguka chini.

Yesu aliwambia, "Mkitumia mafundisho yangu, mtakuwa kama yule mtu wa kwanza." Yesu alimaanisha kwamba maishani kuna ugumu kama dhoruba, lakini tukimfuata, maisha ya mbele kuna kusudi la kudumu. Mwishowe kutakuwa na Ufalme wa Mungu. Mtu asiyefuata Yesu, hatakuwa na tumaini lolote. Mwishowe kutakuwa na mauti tu.

Hebu tujenge maisha yetu kwa mafundisho na mfano kwa Yesu. Mafundisho ya Yesu ni ya maana sana kwa sababu inatwambia vile tunaweza kumpendeza Mungu. Ni lazima tuweke Mungu kwanza, wenzetu wawe wa pili na sisi wenyewe mwisho.

Haja yetu kubwa ni kupata nafasi kwa Ufalme wa Mungu. Hata tena tutafaidika kwa maisha ya sasa kwa sababu Mungu atatulinda. Yesu alitwambia kwamba Mungu anajua wakati mashomoro (mbegu ndogo sana) zinaanguka chini. Kwa hivyo ni zaidi sana Yeye kutulinda kama watoto Wake. Tusishugulikie maisha ya baadaye kwa sababu anatulinda. Atatusaidia kwa shida zetu na kwa majaribu mpaka tufike kwa Ufalme wake.